BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 06 Juni, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

138. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na madai ya wastaafu wa Idara Maalum za SMZ ya kutolipwa stahiki na maslahi tofauti ya kiinua mgongo na pencheni kulingana na matakwa ya kikanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum ya SMZ ya mwaka 2004 na 2007.

(a) Je, ni wastaafu wangapi waliopunjwa ambao wamelipwa na wangapi ambao hawajalipwa tofauti ya mafao yao ya kiinua mgongo na pencheni waliyopunjwa.

(b) Je, kwa nini hadi sasa kuna wastaafu waliopunjwa hawajalipwa tofauti ya mafao yao ya kiinua mgongo na pencheni waliyopunjwa.

(c) Je, ni lini Serikali itatekeleza maamuzi ya Mahakama Kuu ya Zanzibar ya tarehe 22 Novemba, 2016 ya Kesi ya Madai Nam. 30 ya mwaka 2009.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

84. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kufunga hesabu zake kwa kutumia mfumo wa fedha taslimu (Cash basis), na kwa kuwa mfumo huo unaruhusu mapato na matumizi kwa njia ya fedha taslim, na kwa kuwa Serikali inaendelea kuhakiki madeni yanayodaiwa na Serikali kutoka kwa wafanyabiashara na watoa huduma mbali mbali.

(a) Je, kwa nini Taasisi za Serikali zinakopa na kukopesha katika mfumo huu wa fedha taslim.

(b) Je, ni hatua gani zimefikiwa katika kuelekea kwenye Mfumo wa "Accrual Basis (IPSAS)".

Wizara ya Afya:

167. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) zinastahili pongezi kwa jitihada zake katika kuzuia na kupambana na maambukizo ya homa ya Ugonjwa wa Vurusi vya Korona iliyoanza mwaka 2019 (UVIKO-19). Hata hivyo, pamoja na kwamba chanjo ya UVIKO-19 zimekuwa zikitolewa bure Zanzibar, kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu gharama za kufanyia vipimo vya UVIKO-19 (Covid Test) kwa Zanzibar, kiasi kwamba Serikali imeichukulia kama anasa badala ya janga la Kimataifa.

(a) Je, ni vipimo gani vinavyohusiana na Uviko-19 na kwa gharama gani vinafanyika Zanzibar kwa wenyeji na kwa wageni.

(b) Je, ni kwa kiasi gani bajeti ya Serikali imeathirika kimapato na kimatumizi kulikosababishwa na mahitaji ya moja kwa moja ya Uviko-19.

(c) Je, Serikali haioni haja ya kuwaruhusu kufanya vipimo vya Uviko-19 (Covid Test) bila malipo kwa Wazanzibari wanaohitaji kufanya hivyo na ambao walikubali kuchanja kwa hiari.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

112. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa watu wengi katika nchi hii wanatumia tiba mbadala ambapo waganga wengi wa kienyeji pamoja na wauzaji wa dawa za kienyeji hawana utaalamu wa kutosha katika kufanya tiba hiyo, na kwa kuwa katika baadhi ya nchi kuna taasisi maalum zinazojishughulisha na tafiti mbali mbali zinazohusiana na tiba ya mitishamba (herbal medicine research center).

Je, ni lini SMZ kupitia chuo chake kikuu cha SUZA kitaanzisha Kitivo cha Tiba ya Mitishamba (Faculty of Herbal Medicine) ili tiba hiyo iweze kutolewa kitaalamu.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

174. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Sera ya Uchumi wa Buluu ilipokelewa vyema na wananchi walio wengi na iliwajengea matumaini. Hata hivyo, wananchi wengi wamevunjika moyo na mwenendo na utekelezaji wake ikiwemo kudaiwa Ushuru wa Uchumi wa Buluu katika viwanja vya ndege ndani ya Zanzibar pindi wakipita na samaki hata kidogo kwa ajili ya matumizi binafsi.

(a) Je, ni ushuru wa aina gani na wa kiasi gani wananchi wanastahiki kulipa kama Ushuru wa Uchumi wa Buluu.

(b) Je, Serikali haioni kwamba, kuasisi ushuru huu ni kuwazidishia wananchi umasikini na kuwavunja moyo.

(c) Je, ni kiasi gani kimekusanywa kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022 kama makusanyo yatokanayo na Ushuru wa Uchumi wa Buluu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

146. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Inasikitisha kwamba, pamoja na wingi wa mazao yanayotoka katika kijiji cha Mvimbe, zikiwemo karafuu, bado barabara inayounganisha Mvimbe na vijiji vingine si nzuri wala salama.

Aidha, kuna kidaraja ambacho kwa takriban miezi mitatu kila mwaka huwa hakipitiki na huzuia watoto wasiweze kwenda skuli na akina mama kujifungua majumbani kwa shida ya barabara hiyo.

(a) Je, Serikali itaitengeneza lini barabara ya kuendea katika kijiji cha Mvimbe pamoja na kidaraja chake.

(b) Je, wakati Serikali inapanga kuijenga barabara ya kuingilia kijijini Mvimbe, haioni haja ya kuwawekea wananchi, na hasa watoto waendao skuli, kivuko cha muda na kwa haraka ili waweze kuhudhuria skuli hata siku za mvua.

(c) Je, ni lini Serikali iliwahi kuitembelea barabara hii kwa lengo la kuindeleza na kwa nini imetelekezwa.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
06 Juni, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA